BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 20 Juni, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

182. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Pamoja na kuwahamasisha wawekezaji kuja kuekeza Zanzibar, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa wawekezaji hao wanapatiwa mazingira rafiki ya uwekezaji huo.

Je, ni maandalizi gani yaliyokamilika kuwa mazingira rafiki kwa wawekezaji.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

215. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ilikuwa hatua nzuri kwa Serikali mnamo mwaka 2021 kutathmini na kuamua kutozigatua tena sekta zilizogatuliwa kwa majaribio hapo awali. Hata hivyo, katika zoezi hilo la kurejesha sekta zilizokuwa zimegatuliwa awali, kumebakia madeni makubwa ambayo hayakuwahi kulipwa.

(a) Je, ni kiasi gani cha madeni ya wafanyakazi na walimu waliogatuliwa bado hayajalipwa ambayo yalilimbikizwa wakati wakiwa Manispaa na ni lini yamepangwa kulipwa.

(b) Kwa vile Manispaa zilirithi malimbikizo ya madeni yaliyotokana na rambirambi za ufiwa, likizo ya miaka mitatu na stahiki nyengine, je, madeni haya yamefikia kiasi gani kwa upande wa walimu na ni lini yatalipwa na kwa utaratibu upi.

(c) Je, mlundikano wa madeni kwa watumishi waliogatuliwa inaweza kuonekana ni sehemu ya kufeli kwa sera ya ugatuzi Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

179. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa mujibu wa Sheria za Kodi za Zanzibar. Je, Mjasiriamali anaeanza biashara anapaswa kulipa nini.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

211. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wakati dunia ikielekea kwenye ulimwengu wa kidijitali (digitization), inasikitisha kuona kwamba laini za simu za TIGO/ZANTEL zinafungiwa kwa kukosa kutumia vocha ya kukwangua kila mwezi japo mara moja. Aidha, inatia mashaka kuona kwamba wateja waliojiunga na mtandao wa simu wa ZANTEL, sasa wanatambulikana kama wateja wa TIGO bila ya

makubaliano mapya kati ya TIGO, ZANTEL na wateja.

(a) Je, ni sababu ipi inayopelekea wateja kufungiwa laini zao za simu kwa kutotumia vocha ya kukwangua kila mwezi.

(b) Je, Serikali ina kauli gani juu ya mabadiliko ya ZANTEL kuwa TIGO bila ya kuwashirikisha wadau muhimu wakiwemo wateja.

(c) Je, ni upi mfumo na fomula mpya ya hisa za SMZ katika kampuni ya TIGO baada ya kuinunua ZANTEL ambayo SMZ ilikuwa na hisa.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi:</u>**

204. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwa vile inafahamika kwamba ardhi inaendelea kubaki kuwa mali ya umma na sio mali ya Serikali kama inavyotafsiriwa sasa na baadhi ya viongozi.

(a) Je, kwa nini utendaji wa Serikali unaelekea kwenye kuinufaisha zaidi Serikali kuliko wananchi.

(b) Je, kwa nini katika kuwapa ardhi wawekezaji, Serikali inahakikisha kwamba inafaidika zaidi na si kwa kuigawa kodi kwa uwiano mzuri na wenye mantiki baina ya Serikali na mwananchi.

(c) Je, ni upi uwiano wa sasa wa ugawaji wa kodi ya ardhi kwa wawekezaji kati ya Serikali na mwananchi aliyeondolewa kwenye ardhi husika.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

142. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kuhakikisha wananchi wetu wanahamasika katika kukuza kipato chao binafsi, Serikali imeendelea kuwasaidia kuwapa mikopo mbali mbali ili waweze kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Je, kwa kiwango gani mikopo inayotolewa na benki zetu hususan katika kuendeleza Sekta ya Kilimo, inakidhi haja ya mabadiliko ya kilimo.

223. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kauli ya kuwawezesha wakulima kuzalisha na kuyaongezea thamani mazao yanayozalishwa na wakulima wa Zanzibar imekuwa ikirudiwa mara kwa mara, lakini utekelezaji wake kitaifa haujawa wa kiwango cha kuridhisha.

(a) Je, mpango wa Serikali wa kuanzisha viwanda vya kuhifadhia matunda na mboga mboga kitaifa umefikia wapi.

(b) Kwa kuwa moja kati ya sababu zinazopelekea kuongezeka kwa mfumko wa bei ni kuingiza bidhaa nyingi kutoka nje na kusafirisha chache kwenda nje ya nchi. Je, ni upi mpango wa Serikali wa kutafuta masoko ya kuaminika na yenye tija ya bidhaa za wakulima wa Zanzibar.

(c) Je, ni ipi hali ya kupatikana pembejeo za kilimo kwa wakulima kupitia Serikalini kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

231. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Masomo ya Civics, General Studies, History, na Geography ni miongoni mwa masomo ambayo maudhui yake hayamsaidii sana mhitimu, nchi yetu ya Zanzibar wala uchumi wake.

(a) Ili kuendana na mazingira ya Zanzibar na mahitaji ya sasa, Je, Serikali haioni haja ya kuwa na njia mpya ya kuyafundisha masomo hayo ili yalete tija iliyokusudiwa.

(b) Je, Serikali haioni ulazima wa kuwa na utaratibu utakaowafanya wageni wa Zanzibar wenye mpango wa kuishi Zanzibar kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita, kujifunza na kufaulu utamaduni na lugha ya Kiswahili.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha vituo vya majaribio ya uwezo wa Kiswahili (Kiswahili Proficiency Tests (KPT)) ili kutoa huduma hiyo kwa Afrika na dunia kwa jumla.

232. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Bado kuna mkanganyiko wa suala la elimu kuwepo kwenye mambo ya Muungano. Kwa mfano elimu ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita sio jambo la Muungano, lakini shughuli na Baraza la Mitihani la Taifa linalotahini Kidato cha Nne na Sita ni jambo la Muungano; Astashahada (Certificates) na Stashahada (Diploma) sio mambo ya Muungano, lakini wadhibiti wake (NACTVET) wako upande wa pili wa Jamuhuri na si jambo la Muungano.

(a) Je, Serikali imefanya tathmini gani ya karibuni kuhusiana na suala la elimu kuwepo kwake kwenye mambo ya Muungano.

(b) Je, Serikali ina ufumbuzi gani wa suala la elimu kama ni jambo la Muungano, viwango na taasisi zinazoisimamia.

(c) Je, ni vipi Serikali huangalia vipaumbele na aina za kozi zinazohitajika katika vyuo vya Zanzibar, ilhali udhibiti wake hauko kwenye mamlaka ya Zanzibar.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

236. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Majengo mazuri ya hospitali ni hatua moja ya kusogeza huduma bora kwa wananchi. Hata hivyo, wataalamu wa afya wenye viwango ndio ukamilifu wa huduma za afya nchini.

(a) Je, ni kwa nini hospitali na vituo vya afya vingi vina upungufu wa Madaktari, Manesi na Maafisa Afya ilhali wataalamu hao wapo kwa wingi bila ya Serikali kuwapangia kazi hata za kujitolea.

(b) Je, ni ipi takwimu ya idadi na uwanja (Specialization) ya wataalamu wa afya wanohitajika katika hospitali na vituo vya afya Zanzibar baada ya ajira mpya za mwaka 2023.

(c) Je, Serikali imefikia hatua gani na inatumia utaratibu upi wa kuwarasimisha Madaktari wa Tiba Asilia (Traditional Medicine Practitioners).

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

164. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Pamoja na juhudi za Serikali katika kuutangaza utalii kupitia vivutio mbali mbali vilivyopo nchini, uthibitisho wa kuvutika kwao kupitia utaratibu wa watalii hao kurejea nchini kwa miaka mengine, umekuwa mgumu kuuthibitisha.

Je, ni sababu zipi za msingi zinazowafanya watalii wengi wanaotembelea nchi yetu kwa mara ya kwanza kutokurejea tena licha ya kuwa nchi yetu ina vivutio vingi na vizuri vya utalii.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**20 Juni, 2023.**

**(Othman Ali Haji)**
**Kny. KATIBU WA BARAZA**